

**MTEULE ANAPOITIA KATIKA CHANGAMOTO MBALI**  
**MBALI, SIRI PEKEE YA KUVUKA SALAMA NI**  
**KUTULIA NA KUMNGOJA BWANA**  
**MAANDIKO: ZAB. 37:7, ISAYA. 30:15**

**1. UTANGULIZI**

Kama kuna jambo ambalo Bwana amenifundisha mwenyewe saa ninapokuwa napitia changamoto mbali mbali za maisha baada ya kuokoka; Bwana amenifundisha **kutulia** na kumngoja Bwana ili atoe njia yake ya ufumbuzi wa kutatua changamoto hiyo. Roho ya utulivu na ya upole wakati wa changamoto ni siri kubwa na ya pekee sana mbele za Mungu (***Peace and gentle Spirit***). **1Petr. 3:3-4** ni roho yenye thamani sana mbele za Mungu.

- Niliposoma habari za mama huyu, mama mwenye cheo miaka mingi iliyopita nilitamani sana roho hii niwe nayo badala ya kupiga kelele na kulia hovyoy na kupenda kuwasimulia watu changamoto zangu kwa lengo la kutaka kupata msaada kwao. **2 Wafalm. 4:18-37.**
- Kitendo cha mama huyu kufiwa na mtoto wake pekee kilikuwa ni kitendo kizito na jaribu kubwa sana; lakini mwanamke huyu akatulua bila hata kumwambia mume wake maana alifahamu udhaifu wake wala hakuwaambia majirani zake au hata wafanyakazi wake maana alijua fika kwamba hawana ufumbuzi juu ya tatizo hilo. Hili ni somo kubwa sana katika maisha yangu haya ya utumishi. Hadi alipofika kwa Nabii Elisha ndipo akajimwaga na kumwambia yote yaliyompata na Elisha akayapatia ufumbuzi wake!! Unafikiri nini kingetokea kama angepiga yowe kufa!! Elisha angekuta hali gani pale nyumbani!!

2. Mfalme Yehoshefati alijaa roho hii ya upole na utulivu wakati anakabiliana na majeshi ya adui zake. **2 Nyak. 20: 1-30\*12.**

**Yehoshefati alitulia na kuweka msingi wake wa Maombi kwa Mungu kwa kuzingatia kweli tano za msingi sana**

- a. Yehoshafati alifahamu kwa dhati kabisa kwamba Mungu anao uweza juu wa watu wote pamoja na hali zote. **2Nyak. 20: 6-7 (Kumb. 4:37-40). Yer. 32:26-27**

- b. Yehoshefati Mfalme alifahamu kwa kina kwamba Mungu wa Israeli amekuwa mwaminifu kwa watu wake tangu zamani, na anaendelea kuwa mwaminifu hata katika wakati wake **2Nyak. 20:7-9 ( Mwanz. 17:1-8, Kut. 6:6-8)**
- c. Mfalme Yehoshefati pamoja na kuwa na majeshi yake ya kimwili, alifahamu fika kwamba watu wa Mungu msaada wao halisi lazima utoke kwa Mungu na siyo kwa wanadamu. **2Nyak. 20:10-12 ( Zab.46;1-11)**
- d. Mfalme Yehoshafati pia alifahamu kwamba Mungu ahadi zake ni hakika na kweli, akiahidi lazima atatimiza. **2Nyak. 20:14, 17, 20 ( Hes. 23:19) 2Kor. 1:20, Zab. 138:2**
- e. Mfalme Yehoshefati pia alifahamu kwa kina kwamba Mungu anapokuwa yupo katikati yao; Huo ni ushindi na ukombozi mkuu sana. **2Nyak. 20:17-18, Kut. 14:13 na Hes. 14:6-9**  
 Hali hii na ufahamu wa aina hii ndiyo uliomfanya Mfalme Yehoshefati **atulia** hata kama majeshi ya nchi tatu yalikuwa yameungana ili kupigana naye na tunaona mwisho wake ulikuwa ni ushindi mkubwa na Bwana akamstarehesha miaka yote aliyotawala **(25) -2Nyak. 20:29-30**
3. Kutulia ndugu zangu ni siri kubwa sana saa ya changamoto fulani katika maisha haya ( ni kumgoja Bwana akutetee yeye mwenyewe kama Ayubu alivyotulia na kumgoja Bwana **Don't tend to react when you observe a threat situation. Zab. 37:7**
- Mwandishi wa Zaburi hii ni Mfalme Daudi ambaye alijifunza sana kumkabidhi Bwana mambo yake akiamini kwamba atafanya tu. **( Zab. 37:5-6)** yeye alingoja mwaka 13 ili kutawala ingawa tayari alishatiwa mafuta ya kutawala na Nabii Samweli. **1Sam.17:10-13, 2 Samwl. 5:1-5**
  - Wenye haki wanapotulia na kumgoja Bwana; yeye ameahidi kuwapa mahitaji yao na kujibu kilio cha mioyo yao **Filip. 2:13**. Sote tumngojee Bwana kwa saburi na utulivu saa tunapopitia katika changamoto mbalimbali kama Bwana Yesu naye alivyotulia pale msalabani. **Zab. 53:7**

**Na**

**Askofu Dr. L. M. Mwizarubi**

**12/01/2022**

